UTANGULIZI

Kwa kuwa sisi watoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tunatambua kwamba sisi ni sehemu muhimu ya familia zetu, jamii yetu na nchi yetu na kwa ujumla tunazo haki na pia wajibu katika kuendeleza familia zetu, jamii yetu na nchi yetu ili iweze kuwa endelevu na pia kujenga Tanzania na dunia imfaayo kila mtoto.

Na kwa kuwa pia tunatambua na kupongeza jitihada mbalimbali zinazofanyika kitaifa na kimataifa katika kulinda haki na kutetea maslahi ya watoto wote nchini na duniani kote, , tunapongeza kwa dhati jitihada mbalimbali zilizofanyika ikiwemo kupitishwa kwa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Mtoto wa mwaka 1989, Maazimio ya Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali na Mkataba wa Haki na Ustawi wa Mtoto Barani Afrika.

Na kwa kuwa sisi watoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tumeshiriki katika michakato mbalimbali ya kitaifa na kimataifa ikiwemo mkutano wa Bunge la Watoto wa Dunia uliofanyika New York, Marekani mwaka 2001 ambapo watoto waliotuwakilisha walikutana Wilayani Kinondoni, Dar es Salaam na kuazimia kuundwe Baraza la Watoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa msingi huu ili sisi watoto wenyewe tuzitambue na kuzitetea kikamilifu haki zetu na pia kuelimishana sisi wenyewe, familia pamoja na jamii kwa ujumla ili kuelewa haki na wajibu wetu.

Kwa kuwa tunatambua kwa desturi sisi watoto tumekuwa hatushirikishwi katika kufanya maamuzi na kutoa mawazo kuhusu maswala mbalimbali yanayohusu maendeleo yetu, familia zetu na ya jamii kwa ujumla, kwa hiyo basi sisi watoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tunauunda Baraza la Watoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili liweze kuwashirikisha watoto wote na kuwa sauti ya watoto wote na kuchangia kikamilifu katika kuhakikisha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatimiza wajibu wa kujenga mazingira yenye ustawi na yenye kulinda na kutetea ipasavyo haki na maslahi ya mtoto ili kufikia azma ya kuwa na Tanzania na dunia imfaayo kila mtoto ili kuwezesha watoto wote kulelewa vema na kufikia upeo wa uwezo wao kiakili, kiafya, kijamii, kiuchumi na kiutamaduni.

Baraza la Watoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania litaheshimu haki zote za watoto na halitambagua mtoto yeyote kutokana na utaifa, ukabila, pahala anapotokea, maoni yake ya kisiasa, rangi, dini, jinsia, hali yake ya maisha, ulemavu, au kuathirika na virusi vya UKIMWI. Mikataba ya kimataifa kuhusu haki za mtoto ambayo imesainiwa na kuridhiwa na Tanzania ndio itakayokuwa mwongozo rasmi wa shughuli za Baraza. Baraza litafuata sera na taratibu zitakazoundwa na Baraza likisaidiwa na washauri na au walezi katika kuendesha shughuli zake. Sera na taratibu za Baraza zitakuwa wazi kwa watoto wote wa Tanzania, wawakilishi, washauri, walezi na wafadhili.

KIFUNGU CHA KWANZA:JINA, HADHI, ANWANI, DIRA NA UTUME

1.1 **Jina la Katiba:** Katiba hii itajulikana kama Katiba ya Baraza la Watoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

1.2 **Jina la Baraza: ina** rasmi la Baraza litakuwa “Baraza la Watoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.” Kwa ufupi Baraza litajlikana kama ‘BWJMT’

1.3 **Hadhi ya Baraza:** Baraza litakuwa chombo huru kisicho cha Kiserikali kisichegemea wala kushabikia itikadi za kisiasa aua kidini kinachojiendesha chenyewe na kisicholenga kugawana faida.

1.4 **Makao Makuu ya Baraza:** Makao makuu ya Baraza yatakuwa Dar es Salaam, Tanzania. Baraza litakuwa na Ofisi katika kila Mkoa, Wilaya na Kata au Shehia katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

1.5 **Anwani:** Anuani ya Baraza itakuwa S.L.P 21159, Dar es Salaam, Tanzania.

1.6 **Nembo ya Baraza:** Nembo Rasmi ya Baraza itakuwa ni mchoro unaoonyesha watoto wawili, mvulana na msichana, wakiwa wamebeba ramani ya nchi ya Tanzania na kuzungukwa na maneno yafuatayo, kwa Kiswahili na Kiingereza: “Baraza la Watoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania”; “*Junior Council of the United Republic of Tanzania*.”

1.7 **Eneo la kufanya kazi:** Baraza litafanya shughuli zake katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

1.8 **Dira:** Dira ya Baraza ni kuwa chombo imara cha kutetea haki za watoto na kuhamasisha Utekelezaji wa haki hizo na kuelimisha watoto na jamii kuhusu haki na wajibu wa mtoto ili kujenga Tanzania bora na dunia imfaayo kila mtoto.

1.9 **Dhima:** Dhima ya Baraza ni kuwaunganisha na kuwajenga watoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika mazingira bora ya kidemokrasia na kupata uzoefu wa kushiriki na kushirikishwa kikamilifu katika uwakilishi katika michakato mbalimbai ya kisera na ufanyaji maamuzi ili kulinda na kutetea ipasavyo haki na maslahi ya mtoto ili kufikia azma ya kuwa na Tanzania na dunia imfaayo kila mtoto ili kuwezesha watoto kulelewa vema na kufikia upeo wa uwezo wao kiakili, kiafya, kijamii, kiuchumi na kiutamaduni.

1.10 **Usajili:** Baraza litasajiliwa rasmi chini ya sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ili kuondoa utata ieleweke wazi kuwa Baraza litasajiliwa Tanzania Bara na pia litasajiliwa Tanzania Visiwani kwa mujibu wa sheria husika.

1.10 **Lugha rasmi za Baraza:** Lugha zitakazotumika rasmi zitakazotumika katika shughuli za Baraza zitakuwa ni Kiswahili na/au Kiingereza.

KIFUNGU CHA PILI:TAFSIRI

2.0 Katika Katiba hii, isipokuwa tu pale itakapoelezwa vinginevyo, maneno yafuatayo yatatafsiriwa kama inavyoelezwa katika Kifungu hiki:-

"Mtoto" inamaanisha mtu yeyote ambaye ana umri chini ya miaka kumi na minane (18).

'Haki za mtoto' inamaanisha haki na stahili za mtoto zinazotajwa kwenye Katiba hii ni zile zinazotambuliwa na kulindwa na mikataba mbalimbali ya kimataifa inayohusu watoto, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, sheria na sera mbalimbali za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

'Baraza' inamaanisha Baraza la Watoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

KIFUNGU CHA TATU: MADHUMUNI YA BARAZA

3.0 Baraza la Watoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania litakuwa na madhumuni yafuatayo:-

3.1 Kutoa fursa kwa watoto kusikika kupitia mikutano ya kitaifa na kimataifa ya majadiliano kuhusiana na masuala yanayowahusu watoto.

3.2 Kujenga ushirikiano wa karibu kati na baina ya watoto, vyombo vya habari, mashirika yasiyo ya kiserikali na Serikali.

3.3 Kuhakikisha watoto wanapata habari na taarifa sahihi zinazowahusu.

3.4 Kufuatilia utekelezaji wa sera na sheria mbalimbali za nchi zinazowahusu watoto.

3.5 Kuelimisha jamii na watoto juu ya haki na wajibu wa mtoto.

3.6 Kushiriki kwenye harakati za watoto duniani na ufuatiliaji wa mikakati ya Azimio la 'Dunia Iwafaayo Watoto'.

3.7 Kujenga uhusiano na ushirikiano na Mabaraza na Mabunge mbalimbali ya watoto duniani.

3.8 Kukuza na kubadilishana uzoefu na ujuzi na Mabaraza na Mabunge mengine ya watoto duniani katika kupigania haki, wajibu na maendeleo ya mtoto.

3.9 Kutetea haki za watoto na maslahi ya watoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

KIFUNGU CHA NNE: KAZI ZA BARAZA

4.0 Baraza la Watoto la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania litakuwa na kazi zifuatazo:-

4.1 Kutayarisha mikakati ya kukuza ushirikishwaji wa watoto kwenye mambo yanayowahusu watoto katika ngazi zote kuanzia kwenye familia, jamii, serikali za mtaa, kitaifa na kimataifa.

4.2 Kushiriki katika kuandaa, kufuatilia na kutekeleza mikakati ya utendaji kazi kati ya Serikali, mashirika yasiyo ya kiserikali yanayohusika na masuala ya watoto na jamii kwa ujumla katika kuleta mabadiliko yanayofaa kwa maendeleo ya mtoto.

4.3 Kukusanya maoni ya watoto wote Tanzania, kuyachambua na kuyawasilisha katika mamlaka husika na kuyafanyia kazi.

4.4 Kutimiza madhumuni yake mengine kama yanavyoanishwa ndani ya Katiba hii.

4.5 Kufanya kazi kwa karibú na Serikali, Mashirika yasiyo ya Kiserikali na taasisi zingine ikiwemo kuingia katika uwakala ili kutekeleza kwa ufanisi kazi za Baraza pale inapoonekana inafaa.

KIFUNGU CHA TANO:UANACHAMA NA JINSI YA KUJIUNGA

5.1 Uanachama : Uanachama wa Baraza la Watoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania utakuwa wazi kwa watoto wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania bila ubaguzi wowote.

5.1.1 Haki ya kila mtoto kuwa mwanachama: Watoto wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wanayo haki ya kuwa wanachama wa Baraza isipokuwa tu umri wa mwanachama wa Baraza usizidi miaka kumi na nane (18).

5.1.2 Aina za uanachama: Baraza litakuwa na wanachama wa aina tatu (3) ambao ni:-

a. Wanachama waanzilishi
b. Wanachama wa Kawaida
c. Wanachama wa kushirikishwa

5.1.3 Mwanachama mwaanzilishi ni mtoto yeyote mwenye umri usiozidi miaka kumi na na nane (18) ambaye ameshiriki katika mchakato wa kuunda na kusajili Baraza.

5.1.4 Mwanachama wa kawaida ni mtoto yeyote mwenye umri usiozidi miaka kumi na na nane (18)ambaye atajiunga na Baraza baada ya kusajiliwa kwa mujibu wa utaratibu wa kujiunga uanachama ambao utakuwa umewekwa na Katiba hii.

5.1.5 Mwanachama wa kushirikishwa ni mtoto yeyote mwenye umri usiozidi miaka kumi na na nane (18) ambaye atajiunga na Baraza lakini si raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na atakuwa na haki zote isipokuwa tu kupiga kura au kuchaguliwa kuwa kiongozi.

5.2 JINSI YA KUJIUNGA

5.2.1 **Fomu ya maombi:** Mtoto yeyote mwenye sifa za kujiunga kuwa mwanachama wa Baraza atajaza fomu maalum ya maombi ya uanachama na kuwasilisha kwa Katbu wa Baraza katika ngazi ya Klabu, Kata au Shehia, Wilaya au Mkoa.

5.2.2 **Kujadiliwa ombi la uanachama na Kamati ya Wilaya au Mkoa na Mkutano Mkuu:** Kamati ya Wilaya au Mkoa itajadili na kutoa mapendekezo ya ama kukubali kumwingiza au kumkatalia uanachama mwombaji yeyote kutokana na kutimiza au kutotimiza sifa za uanachama. Mapendekezo ya Kamati yatawasilishwa katika Mkutano Mkuu wa Wilaya au Mkoa na kisha kuwasilisha taarifa ya wanachama wapya kwenye kikao cha Kamati Kuu ya Baraza ambayo itawasilisha orodha ya wanachama wapya kwenye Mkutano Mkuu wa Baraza la Watoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

5.3 **SIFA ZA UANACHAMA**

Mtoto yeyote mwenye umri usiozidi miaka kumi na nane ambaye anaishi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anazo sifa za kuomba kuwa mwanachama wa Baraza. Isipokuwa ieleweke wazi kuwa mtoto asiye raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anayo haki ya kuwa tu mwanachama mshiriki na kamwe si mwanachama wa kawaida.

5.4 **HAKI NA WAJIBU WA KILA MWANACHAMA**

5.4.1 **Haki za mwanachama wa Baraza:** Kila mwanachama wa Baraza atakuwa na haki za uanachama zifuatazo:-

a. kushiriki kikamilifu katika shughuli za Baraza
b. kuchagua au kchaguliwa kuwa mwakilishi na au kiongozi katika ngazi mbalimbali za Baraza.
c. Kupata taarifa mbalimbali zihusianazo na uendeshaji wa Baraza na maswala mbalimbali yanayomhusu mtoto.
d. Kutoa maoni katika vyombo mbalimbali vya Baraza ambavyo yeye ni mjumbe.

5.4.2 **Wajibu wa Mwanachama wa Baraza:** Kila mwanachama wa Baraza atakuwa na wajibu ufuatao:-

a. Kulinda na kutetea Katiba ya Baraza.
b. Kushiriki kikamilifu katika shughuli mabalimbali za Baraza katika ngazi husika.
c. Kuhudhuria mikutano ya Baraza katika ngazi husika.

Ieleweke wazi kuwa wanachama hawatakuwa na wajibu wa kulipa kiingilio cha uanachama, ada ya uanachama na au michango mingine yeyote.

5.5 **KUKOMA KWA UANACHAMA**

Uanachama wa Baraza utakoma iwapo mjawapo kati yafutayo litatokea:-

(a) Kujiuzulu au kujitoa uanachama mwenyewe.
(b) Kuondolewa au kufukuzwa uanachama na Mkutano Mkuu katika Ngazi husika.
(c) Kutohudhuria Mikutano mikuu mitatu (3) ya Baraza mfululizo bila taarifa yoyote.
(d) Kutimiza umr wa miaka kumi na nane(18).
(e) Kufariki dunia.

KIFUNGU CHA SITA: UWAKILISHI WA MIKOA KATIKA BARAZA LA WATOTO WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

6.1 **Kuundwa kwa Baraza:** Kutakuwa na Baraza la Watoto la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania litakaloundwa na wawakilshi kutoka mikoa yote ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uwiano uliosawa, isipokuwa tu kwa Mkoa wa Dar es Salaam.

6.2 Uwakilishi wa Mikoa katika Baraza

6.2.1 **Idadi ya wawakilishi katika Baraza:** Baraza litakuwa na wawakilishi wapatao sabini (70) ambao watatoka mikoa yote ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuzingatia jinsi.

6.2.2 **Idadi ya wawakilishi kwa kila Mkoa:** Kila mkoa utatoa wawakilishi wawili (2), isipokuwa Mkoa wa Dar es Saalaam ambao utawakilishwa na wawakilishi sita ambapo kila Wilaya ya mkoa wa Dar es Salaam itatoa wawakilishi wawili

6.2.3 **Muda wa uongozi:** Wajumbe wa Baraza watakuwa madarakani kwa kipindi cha miaka miwili tu.

6.2.4 **Ukomo wa uongozi:** Mjumbe wa Baraza aliyemaliza muda wake wa uongozi kwa kipindi cha miaka miwili ya mwanzo anaweza kuchaguliwa tena kwa kipindi cha pili cha uongozi lakini hataweza kuchaguliwa kuwa mjumbe au kiongozi kwa vipindi zaidi ya viwili.

6.3 Aina ya Uwakilishi

6.3.1 **Wawakilishi wa Mikoa:** Wawakilishi kutoka kila mkoa ambao watachaguliwa na watoto katika mikoa wanakotokea.

6.3.2 **Wawakilishi wa makundi maalum:** Wawakilishi walioteuliwa kutoka katika makundi maalum, kwa mfano watoto walio katika mazingira magumu viziwi na mabubu, wasioona, walemavu wa viungo, albino, yatima, watoto wenye mtindio wa akili, viziwi wasioona,waathirika wa VVU/UKIMWI, n.k isipokuwa tu idadi ya wawakilishi hawa wa makundi maalum isizidi wawakilishi kumi na nne (14).

6.4 Sifa za mwakilishi wa Baraza.

Bila ya kuathiri masharti yaliyomo katika kifngu hiki, mtoto yeyote atakuwa na sifa za kustahili kuchaguliwa kuwa Mwakilishi endapo-

6.4.1 Ni raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye umri wake ni chini ya miaka 18.

6.4.2 Amechaguliwa na watoto wenzake katika Mkoa anaouwakilisha.

6.4.3 Mwakilishi sio lazima awe na uzoefu katika masuala ya haki za watoto bali aonyeshe uwezo wa kuweza kuwawakilisha watoto wenzake.

6.5 UCHAGUZI WA WAWAKILISHI

6.5.1 Watoto katika kila Mkoa watafahamishwa na mwezeshaji wa uchaguzi juu ya taratibu za uchaguzi na maelezo kuhusu Katiba na Baraza la Watoto la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

6.5.2 Wawakilishi wa Baraza watachaguliwa miongoni mwa watoto walioomba au waliopendekezwa na watoto wenzao.

6.5.3 Mjumbe anayeomba nafasi ya uwakilishi itampasa atoe sababu za kuomba nafasi hiyo kwa kujieleza mbele ya kikao kitakachoitishwa na mwezeshaji wa uchaguzi kwa ajili hiyo.

6.5.4 Wajumbe waliopendekezwa na watoto wenzao wanaweza kujieleza lakini pia mtoto aliyependekeza jina la mjumbe anaweza kuelezea ni kwa nini mtoto huyo anafaa kuwa mwakilishi.

6.5.5 Uchaguzi wa wawakilishi wa Baraza utasimamiwa na Kamati ya Uchaguzi itakayochaguliwa kwa wakati huo.

6.5.6 Uchaguzi wa wawakilishi wa Baraza utafanyika kwa kupiga kura ya siri. Mjumbe ambaye atashinda kwa kura nyingi yaani zaidi ya asilimia 50, ndiye atakuwa ameshinda. Iwapo kura zitakuwa zimefungana au hakuna mgombea aliyepata zaidi ya asilimia 50 ya kura uchaguzi utarudiwa hadi apatikane au wapatikane washindi.

6.5.7 Uchaguzi wa wawakilishi wa Mkoa katika Baraza la Watoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania au katika Mabaraza ya Mikoa, Wilaya na Kata au Shehia utazingatia usawa wa jinsia.

6.6 HAKI ZA MWAKILISHI KATIKA BARAZA

Mwakilishi wa Baraza atakuwa na haki zifutazo katika uendeshaji wa shughuli za Baraza:-

6.6.1 Kupiga na au kupigiwa kura.

6.6.2 Kuhoji, kuhojiwa na kukosolewa.

6.6.3 Kuuliza swali lolote kuhusiana na utendaji kazi wa Kamati za Baraza.

6.6.4 Kupata taarifa sahihi kuhusiana na Baraza.

6.7 WAJIBU WA MWAKILISHI

Mwakilishi wa Baraza atakuwa na wajibu ufuatao:-

6.7.1 Kuendeleza na kutetea haki na wajibu na maendeleo ya watoto.

6.7.2 Kuhudhuria vikao vya Baraza.

6.7.3 Kutoa mawazo na kusikiliza na kuheshimu mawazo ya watoto wenzake.

6.7.4 Kutekeleza kazi nyingine yoyote ile kama inavyotakiwa kwa mujibu wa Katiba hii.

6.8 KUSIMAMISHWA, KUFUKUZWA NA AU KUREJESHEWA UWAKILISHI

6.8.1 Mwakilishi yoyote anaweza kusimamishwa, kufukuzwa uwakilishi pale atakapokiuka misingi ya Katiba hii.

6.8.2 Kukoma kuwa mjumbe wa Baraza kutategemea sifa zilizoainishwa katika kifungu cha saba (7) cha Katiba hii ikiwa ni pamoja na;

(i) Kumalizika kwa muda wa uwakilishi.

(ii) Kifo.

(iii) Kutimiza umri wa miaka kumi na nane (18).

(iv) Kutokuhudhuria vikao vitatu mfululizo bila ya taarifa maalum.

KIFUNGU CHA SABA: MUUNDO WA BARAZA

NGAZI ZA BARAZA LA WATOTO WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

7.1 Baraza la Watoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania litakuwa na ngazi zifuatazo katika kuendesha shughuli zake:-

7.1.1 Ngazi ya Taifa
7.1.2 Ngazi ya Mkoa
7.1.3 Ngazi ya Wilaya
7.1.4 Ngazi ya Kata au Shehia

7.1.5 Klabu au Baraza la Watoto katika shule au vituo ambapo watoto wanakusanyika pamoja kwa muda mwingi au kuishi pamoja pale idadi yao inapokuwa ni zaidi ya watoto ishirini (20).

7.2 Kwa ujumla, shughuli na mamlaka ya Baraza yatatekelezwa na wanachama au wawakilishi wao kupitia mikutano, vikao na vyombo vilivyoundwa na Katiba hii ili kusimamia na kutekeleza shughuli za Baraza katika ngazi mbalimbali.

7.3 Kwa ajili ya kuhakikisha uwiano mwaafaka kijinsia, kila chombo au mkutano au kikao kinachoundwa kwa mujibu wa Katiba hii, kitazingatia uwiano wa jinsi katika uchaguzi wa viongozi au wawakilishi au wajumbe wa chombo hicho.

KIFUNGU CHA NANE:MUUNDO WA UONGOZI WA BARAZA KATIKA NGAZI YA TAIFA

8.1 Kutakuwa na vyombo na vikao vifuatavyo katika kutekeleza mamlaka na shughuli za Baraza katika Ngazi ya Taifa:-

8.1.1 Mkutano Mkuu wa Baraza la Watoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
8.1.2 Kamati Kuu
8.1.3 Sekretariati.
8.1.4 Bodi ya Washauri.
8.1.5 Bodi ya Wadhamini.

8.2 MKUTANO MKUU

8.2.1 **Mkutano Mkuu:** Kutakuwa na Mkutano Mkuu wa Baraza la Watoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambao utakaofanyika mara moja kwa mwaka.

8.2.2 Mkutano Mkuu utakuwa ndicho chombo cha juu zaidi na cha mwisho katika kufanya maamuzi juu ya maswala mbalimbali ya Baraza.

8.3 **Kazi za Mkutano Mkuu:** Mkutano Mkuu utafanya shughuli zifuatazo:-

a. Kupokea, kujadili, kukubali au kukataa taarifa ya maendeleo na utekelezaji wa shughuli za Baraza kila mwaka.
b. Kupitisha mpango kazi na bajeti kwa mwaka unaofuata.
c. Kupokea taarifa ya mkaguzi wa hesabu za Baraza kila mwaka.
d. Kufanya uchaguzi na uteuzi wa wajumbe wa Bodi ya Wadhamini na pia wajumbe wa Bodi ya Ushauri.

e. Kupitisha marekebisho au mabadiliko ya Katiba ya Baraza la Watoto la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
f. Kupokea na kuthibitisha orodha ya wanachama wapya itakayowakilishwa na Mabaraza ya Mkoa na Wilaya.
g. Kuwajibisha wanachama, viongozi au wajumbe wa Kamati Kuu waliokiuka malengo, madhumuni, Katiba na maadili ya Baraza.
h. Kutoa maelekezo juu ya mipango, mikakati na utekelezaji wa mamlaka na shughuli za Baraza kwa vyombo vingine vya Baraza katika ngazi zote.
i. Kuteua mkaguzi wa mahesabu ya Baraza la Watoto wa Jamhuri ya Muungano kwa mwaka unaofuata.
j. Kufanya jambo jingine lolote ambalo kwa kawaida hufanywa na Mkutano Mkuu.

8.4 **Wajumbe wa Mkutano Mkuu:** Mkutano Mkuu utahudhuriwa na wajumbe wote wa Kamati Kuu na wawakilishi wanaounda Baraza la Watoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutoka Mikoa yote na makundi maalum yaliyoainishwa kwa mujibu wa Katiba hii.

8.5 **Wajumbe waalikwa kuhudhuria Mkutano Mkuu:** Kamati Kuu inaweza kualika wajumbe waalikwa ili wahudhurie Mkutano Mkuu kadiri itakavyoona inafaa. Isipokuwa, ieleweke wazi kuwa waalikwa hawatakuwa na haki ya kupiga kura au kuchaguliwa katika nafasi za uongozi.

8.6 **Uendeshaji wa shughuli na ufanyaji maamuzi katika Mkutano Mkuu:** Mkutano Mkuu utakuwa halali pale tu utakapohudhuriwa na na wajumbe wasiopungua asilimia sabini na tano (75%) ya ya wajumbe wote.

8.6.2 Mkutano Mkuu unaweza kukasimu baadhi ya mamlaka yake kwa Kamati Kuu kwa jambo ambalo umeanza kulifanyia kazi lakini haujalitolea maamuzi pale utakapoona sio busara kusubiri hadi kikao kingine cha Mkutano Mkuu.

8.6.3 Taarifa ya maandishi ya kuitisha Mkutano Mkuu itatolewa walau siku thelathini (30) kabla ya kikao cha Mkutano Mkuu kufanyika.

8.6.4 Taarifa ya wito wa kuhudhuria kikao cha Mkutano Mkuu itaonyesha tarehe, muda na mahali ambapo Mkutano Mkuu utafanyika.

8.6.5 Taarifa ya kuitisha Kikao cha Mkutano Mkuu itatolewa na Katibu na kuwasilishwa kwa Makatibu wa Baraza katika Ngazi ya Mkoa.

8.6.6 Katibu wa Baraza katika Ngazi ya Mkoa atasambaza Taarifa ya kuitishwa kwa Mkutano Mkuu kwa wajumbe wote walio katika Mkoa wake.

8.6.7 Kila mjumbe wa Mkutano Mkuu anayehudhuria kikao halali atakuwa na kura moja ya siri. Iwapo kura zitafungana kati ya makundi mawili; Mwenyekiti atakuwa na kura ya uamuzi.

8.6.8 Maamuzi ya Baraza yatapitishwa kwa maelewano na pale inapolazimu kwa kupigiwa kura ya siri.

8.6.9 Uamuzi wa Baraza utakuwa umepita kama utapata asilimia hamsini ya kura zote za Wajumbe waliopo na wanaoruhusiwa kupiga kura, isipokuwa tu iwapo uamuzi unaofanywa unahusu marekebisho au mabadiliko ya

katiba au uchaguzi ambapo taratibu zilizoelezwa katika vifungu husika zitatumika.

8.7 **MKUTANO MKUU WA DHARURA**

8.7.2 **Mkutano Mkuu wa dharura:** Mkutano Mkuu wa Dharura wa Baraza la Watoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania utaitishwa wakati wowote kunapotokea jambo la dharura ambalo linahitaji kufanyiwa maamuzi ya haraka na Mkutano Mkuu.

8.7.3 **Azimio la kuitisha Mkutano Mkuu wa Dharura:** Mkutano Mkuu wa Dharura utaitishwa na wawakilishi wa Mikoa iwapo theluthi moja ya wajumbe halali wa Mkutano Mkuu kutoka walau Mikoa kumi (10) ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wataafiki kwa kuwasilisha Azimio la maandishi lenye majina; anwani na saini zao na lenye kutaja ajenda za kikao cha Mkutano Mkuu wa Dharura; litakapowasilishwa kwa Katibu kwa lengo la kumtaka aitishe kikao cha Mkutano Mkuu wa Dharura mara moja.

8.7.4 Taarifa ya wito wa kuhudhuria Mkutano Mkuu wa Dharura itatolewa si chini ya siku thelathini (30) kabla ya kikao cha Mkutano Mkuu wa Dharura kufanyika.

8.7.5 **Kazi ya Mkutano Mkuu wa Dharura:** Mkutano Mkuu wa Dharura utakapoitishwa na idadi ya wajumbe kutimia utafanya shughuli zake kama Mkutano Mkuu wa kawaida na kutoa maamuzi, maagizo au maelekezo kwa Kamati Kuu baada ya kujadili ajenda zilizowasilishwa katika Azimio la kuitisha Mkutano huo. Ieleweke wazi kuwa Mkutano Mkuu wa Dharura hautakuwa na mamlaka ya kujadili na kutolea maamuzi, maagizo au maelekezo ajenda yeyote au jambo jingine lolote mbali ya ajenda iliyoainishwa katika wito wa kuitishwa kwa Mkutano Mkuu huo wa Dharura.

KIFUNGU CHA TISA: KAMATI KUU YA BARAZA LA WATOTO WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

10.1 **Kamati Kuu:** Kutakuwa na Kamati Kuu ya Baraza la Watoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

10.2 **Wajumbe wa Kamati Kuu** Kamati Kuu itakuwa na wajumbe kumi (10) na itaundwa na viongozi wa Baraza katika ngazi ya Taifa wafuatao:

10.2.1 Mwenyekiti.
10.2.2 Makamu Mwenyekiti.
10.2.3 Katibu.

10.2.4 Mweka Hazina.
10.2.5 Wajumbe sita (6).

10.3 **Kazi za Kamati Kuu:** Kamati Kuu itafanya kazi zifuatazo

10.3.1 Kutunga taratibu na sera zote za Baraza.

10.3.2 Kutekeleza maamuzi yatakayotolewa na Mkutano Mkuu na pia ushauri utakaotolewa na Bodi ya Ushauri, Bodi ya Wadhamini au Mlezi au Walezi wa Baraza.

10.3.3 Kuunda kamati ndogondogo kutegemeana na mahitaji kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za mbalimbali mahsusi za Baraza.
10.3.4 Kupitisha na kupendekeza mambo na taarifa mbalimbali zinzohusu hali na ustawi wa watoto wa Tanzania.
10.3.5 Kufuatilia masuala, maamuzi na maandalizi yanayopaswa kufanywa kwa ajili ya Baraza katika sehemu mbalimbali ikiwemo serikalini, mashirika yasiyo ya kiserikali na taasisi zingine.
10.3.6 Kutoa muhtasari wa shughuli zote na maamuzi/majukumu yaliyopaswa kutekelezwa mbele ya Baraza la Watoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
10.3.7 Kupanga na kusimamia shughuli zote za Baraza za kiutawala na pia shughuli zote za kamati ndogo za Baraza.
10.3.8 Kufuatilia masuala, maamuzi na maandalizi yanayopaswa kufanywa kwa ajili ya Baraza katika sehemu mbalimbali ikiwemo Serikalini na kwa mashirika yasiyo ya kiserikali na taasisi nyinginezo.
10.3.9 Kuwajibika kwa Baraza la Watoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
10.3.10 Kusimamia matumizi ya fedha na rasilimali mbalimbali za Baraza.
10.3.11 Kupendekeza jina la mkaguzi wa mahesabu na kuliwasilisha mbele ya wajumbe Mkutano Mkuu wa Baraza ili kuidhinishwa.
10.3.12 Kumsimamisha kiongozi yeyote mwakilishi au mwanachama yeyote anayetuhumiwa kukiuka Katiba na maadili ya Baraza na baada ya kupitia kwa kina tuhuma hizo na kumpa mtuhumiwa haki ya kusikilizwa na kuwasilisha mapendekezo mbele ya Mkutano Mkuu ama umfukuze uongozi au imrejeshee uongozi mtuhumiwa.
10.3.13 Kupanga kalenda ya vikao vyote vya Baraza la Watoto la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwa ni pamoja na vikao vya:-

a. Mkutano Mkuu wa Baraza la Watoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
b. Bodi ya Ushauri
c. Bodi ya Wadhamini
d. Kamati Kuu
e. Mikutano mingineyo kama itakavyoonekana inafaa.

10.4 **Vikao vya Kamati Kuu:** Kamati Kuu ya Baraza la Watoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itakutana mara nne kwa mwaka yaani kila baada ya miezi mitatu (3).

10.5 Wajumbe wa Kamati Kuu wanapaswa kupewa taarifa ya mkutano sio chini ya siku thelathini (30) kabla ya mkutano wenyewe kufanyika.

10.6 Kila mjumbe wa Kamati Kuu anayehudhuria kikao halali atakuwa na kura moja ya siri. Iwapo kura zitafungana kati ya makundi mawili; Mwenyekiti atakuwa na kura ya uamuzi.

10.7 **Ufanyaji maamuzi katika Kamati Kuu:** Maamuzi ya Kamati Kuu ya Baraza la Watoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yatapitishwa kwa maelewano na pale inapolazimu kwa kupigiwa kura ya siri. Endapo kura zitafungana Mwenyekiti atakuwa na kura ya uamuzi.

10.8 Uamuzi wa Kamati Kuu ya Baraza la Watoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania utakuwa umepita kama utapata asilimia hamsini ya kura zote za Wajumbe waliopo na wanaoruhusiwa kupiga kura, isipokuwa tu iwapo uamuzi unaofanywa unahusu marekebisho au mabadiliko ya katiba au uchaguzi ambapo taratibu zilizoelezwa katika vifungu husika zitatumika.

10.9 Kamati Kuu inaweza kukasimu baadhi ya kazi zake mahsusi kwa Mwenyekiti au Katibu inapoona sio busara kusubiri hadi kikao kingine cha Kamati Kuu.

KIFUNGU CHA KUMI: SEKRETARIATI YA BARAZA LA WATOTO WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

10.1 Sekretariati: Kutakuwa na Sekretariati ya Baraza la Watoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo itakuwa na wajibu wa kutekeleza shughuli za kila siku chini ya usimamizi wa Kamati Kuu.

10.2 Sekretariati itawajibika kwa Kamati Kuu ya Baraza la Watoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

10.3 Wajumbe wa Sekretariati: Sekretariati itaundwa na Mratibu pamoja na wafanyakazi wengine ama wa kudumu au wa kujitolea kadri itakavyoonekana inafaa.

10.4 Kazi za Sekretariati: Sekretariati itafanya kazi zifuatazo:-

(a) Kuandaa na kutekelezaji wa shughuli za kila siku za Baraza.

(b) Kubuni, kuandaa, kuitekeleza na kuitathmini mipango mbalimbali ya maendeleo ya Baraza kulingana na malengo na madhumuni ya Baraza kama yalivyoainishwa katika Katiba hii.

(c) Kufuatilia, kukagua na kutathmini utekelezaji wa shughuli, mipango na miradi yote ya Baraza katika ngazi zote.

(d) Kuandaa vikao na mikutano yote ya Baraza katika Ngazi ya Taifa kwa maagizo na Kamati Kuu.

(e) Kuandaa kalenda ya Mkutano Mkuu wa Baraza katika ngazi ya Taifa na vikao vya Bodi ya Ushauri, Bodi ya Wadhamini na Kamati Kuu kila mwaka kwa maagizo ya Kamati Kuu.

(f) Kutoa huduma mbalimbali za kitaalamu na za kiutawala kwa ngazi zote za Baraza kadri itakavyohitajika katika kupanga na kutekeleza shughuli za Baraza.

(g) Kufanya shughuli yeyote itakayoagizwa na Kamati Kuu.

KIFUNGU CHA KUMI NA MOJA: BODI YA USHAURI

11.1 Bodi ya Ushauri: Kutakuwa na Bodi ya Washauri wa Baraza la Watoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo idadi yao itaundwa na wajumbe kumi (10).

11.2 Wajumbe wa Bodi ya Ushauri: Wajumbe wa Bodi ya Ushauri watateuliwa na Mkutano Mkuu ambapo wajumbe watakaoteuliwa watakuwa ni:

11.2.1 Mkurugenzi anayehusika na maendeleo ya mtoto katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania au mwakilishi wake.

11.2.2 Mkurugenzi anayehusika na masuala ya wanawake na watoto katika Serikali ya Mapinduzi Zanzibar au mwakilishi wake.

11.2.3 Kamishna anayeshughulika na masuala ya ustawi wa jamii katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania au mwakilishi wake.

11.2.4 Mkurugenzi anayeshughulika na masuala ya ustawi wa jamii katika Serikali ya Mapinduzi Zanzibar au mwakilishi wake.

11.2.5 Mwenyekiti wa Kamati Kuu ya Baraza la Watoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye atakuwa amemaliza muda wake karibuni.

11.2.6 Katibu wa Kamati Kuu ya Baraza la Watoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye atakuwa amemaliza muda wake karibuni.

11.2.7 Mweka Hazina wa Kamati Kuu ya Baraza la Watoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye atakuwa amemaliza muda wake karibuni.

11.2.8 Mwakilishi kutoka taasisi za Umoja wa Mataifa.

11.2.9 Mwakilishi kutoka shirika moja lisilo la kiserikali linaloshughulika na masuala ya watoto la ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (local NGO).

11.2.10 Mwakilishi wa shirika moja lisilo la kiserikali la kimataifa linaloshughulika na maswala ya watoto lenye kufanya kazi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

11.3 Mikutano ya Bodi ya Ushauri: Bodi ya Ushauri itakutana mara tatu kwa mwaka yaani mara moja kila baada ya miezi minne (4). Lakini Bodi ya Ushauri inaweza kukutana kwa ajili ya kikao cha dharura wakati wowote itakapohitajika.

11.4 Katika kikao cha kwanza Bodi ya Ushauri itachagua miongoni mwake Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Katibu.

11.5Kazi za Bodi ya Ushauri: Bodi ya Ushauri itafanya kazi zifuatazo:-

(a) Kupokea, kutathmini, kujadiliana na kushauriana juu ya maswala mbalimbali ya ustawi na uendeshaji wa Baraza la Watoto la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika ngazi zote kama yatakavyowasilishwa na Kamati Kuu.
(b) Kushauri namna bora za kuendesha shughuli za Baraza la Watoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pale inapohitajika bila kubadili mipango iliyopangwa na Baraza**.**
(c) Kutathmini uadilifu na utawala bora katika Ngazi zote za Baraza katika kusimamia na kutekeleza malengo na madhumuni yaliyoainishwa katika Katiba hii.
(d) Kushauri jinsi ya kuboresha mahusiano na mawasiliano kati ya Ngazi mbalimbali za Baraza.
(e) Kushughulikia na kushauri ama kutatua migogoro itakayojitokeza katika uendeshaji wa shughuli za Baraza katika ngazi zote.
(f) Kufanya jambo jingine lolote kama itakavyoagizwa na Mkutano Mkuu au kuombwa na Ngazi ya Taifa, Mkoa au Wilaya.

11.6Uitishaji wa vikao na ufanyaji maamuzi katika Bodi ya Ushauri: Kikao cha Bodi ya Ushauri kitaitishwa kwa taarifa ya maandishi inayooonyesha siku, mahali na ajenda za kikao itakayotolewa na kusambazwa kwa wajumbe wote wa Bodi ya Ushauri walau siku kumi na nne kabla ya Kikao.

11.7 Mahudhurio yanayowezesha kufanyika kwa kikao cha Bodi ya Ushauri itakuwa ni zaidi ya asilimia sabini na tano (75%) ya ya wajumbe wote.

11.8 Ushauri wa Bodi utafanyika kwa maelewano na Iwapo itahitajika kupiga kura za siri ili kufikia uamuzi wa jambo lolote katika kikao kila mjumbe atakuwa na kura moja. Iwapo kura zitafungana kati ya makundi mawili, Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri atakuwa na kura ya uamuzi.

11.9 Uamuzi wa Bodi ya Ushauri utakuwa umepita kama utapata zaidi ya asilimia hamsini ya kura zote za Wajumbe waliopo na wanaoruhusiwa kupiga kura.

KIFUNGU CHA KUMI NA MBILI: BODI YA WADHAMINI WA BARAZA LA WATOTO LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

12.1Bodi ya Wadhamini: Kutakuwa na Bodi ya Wadhamini wa Baraza la Watoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo itasajiliwa kwa mujibu wa

sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika sehemu zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yaani Tanzania Bara na Tanzania Visiwani.

12.2 **Wajumbe wa Bodi ya Wadhamini:** Bodi ya Wadhamini itaundwa na wadhamini watano (5) ambao watakuwa ni wawakilishi wa Serikali, Umoja wa Mataifa, Mashirika yasiyo ya Kiserikali yanayojishughulisha na watoto na taasisi nyingine kama itakavyoonekana inafaa.

12.3 Wajumbe wa Bodi ya Wadhamini watapendekezwa na Kamati Kuu na kuidhinishwa na mkutano mkuu wa Baraza la Watoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**.**

12.4 **Kazi za Bodi ya Wadhamini:** Bodi ya Wadhamini itafanya kazi zifuatazo:-

a. Kusimamia na kulinda mali na rasilimali za Baraza la Watoto wa Jamhuri ya Muugano wa Tanzania.

b. Kushtaki na kushtakiwa kwa niaba ya Baraza la Watoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

c. Kusimamia uingiaji wa mikataba na taasisi zingine na uwekezaji wa mali na rasilimali za Baraza.

d. Kufungua na kuendesha akaunti za Baraza la Watoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika mabenki na taasisi mbalimbali za fedha.

e. Kufanya jambo jingine lolote ambalo kwa kawaida hufanywa na Bodi ya Wadhamini.

5. Baraza pamoja na Bodi ya Wadhamini litafanya kazi kwa karibu kabisa na watendaji wengine kwenye sekta ya maendeleo ya mtoto hususan Serikalini, mashirika yasiyo ya kiserikali, mashirika ya kidini na wengineo.

12.5 **Ukomo wa kuwa mjumbe wa Bodi ya Wadhamini:** Kamati Kuu inaweza kupeleka mapendekezo kwa Mkutano Mkuu ya kumwondoa madarakani mdhamini yeyote baada ya kupiga kura za asilimia sabini. Mkutano Mkuu ukiridhia mapendekezo ya Kamati Kuu utamwondoa mara moja Mdhamini kutoka katika wadhifa huo.

12.6 Mdhamini pia anaweza kuondolewa madarakani na Mkutano Mkuu wa Baraza la Watoto wa Jamhuri ya Muungao wa Tanzania endapo-

a. Itathibitika ametumia vibaya madaraka; au
b. Ameathiri utendaji wa kazi, malengo au heshima ya Baraza.

12.7 Uamuzi wa kumwondoa madarakani mdhamini utafikiwa baada ya mdhamini huyo kupewa nafasi ya kutoa maelezo ya kujitetea.

12.8 Mdhamini anaweza kujiuzulu kwa kutoa taarifa ya maandishi ya siku sitini kwa Kamati Kuu.

12.9 Mkutano wa wadhamini utakuwa halali kama ukihudhuriwa na wadhamini wasiopungua watatu (3).

12.10 **Uitishaji wa vikao na ufanyaji maamuzi katika Bodi ya Wadhamini:** Kikao cha Bodi ya Wadhamini kitaitishwa kwa taarifa ya maandishi inayoonyesha siku, mahali na ajenda za kikao itakayotolewa na kusambazwa kwa wajumbe wote wa Bodi ya Udhamini walau siku kumi na nne (14) kabla ya Kikao.

12.11 Mahudhurio yanayowezesha kufanyika kwa kikao cha Bodi ya Udhamini itakuwa ni zaidi ya asilimia sitini (60%) ya ya wajumbe wote.

12.12 Uamuzi wa Bodi utafanyika kwa maelewano na Iwapo itahitajika kupiga kura za siri ili kufikia uamuzi wa jambo lolote katika kikao kila mjumbe atakuwa na kura moja. Iwapo kura zitafungana kati ya makundi mawili, Mwenyekiti wa Bodi ya Udhamini atakuwa na kura ya uamuzi.

12.13 Uamuzi wa Bodi ya Udhamini utakuwa umepita kama utapata zaidi ya asilimia hamsini ya kura zote za Wajumbe waliopo na wanaoruhusiwa kupiga kura.

KIFUNGU CHA KUMI NA TATU: UTARATIBU WA UCHAGUZI WA VIONGOZI NA WAJUMBE WA KAMATI KUU YA BARAZA LA WATOTO WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, KAMATI ZA MIKOA, WILAYA, KATA, SHEHIA NA KLABU

13.1 Katika kila ngazi ya Baraza la Watoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania watachaguliwa viongozi wakuu wa Baraza ambao watakuwa ni:

1. Mwenyekiti
2. Makamu Mwenyekiti
3. Katibu
4. Mweka Hazina na
5. Wajumbe wa Kamati Kuu wasiozidi sita (6).

13.2 Viongozi hawa watachaguliwa katika Mkutano Mkuu wa ngazi husika ya Baraza ambapo mkutano Mkuu utachagua wajumbe wasiozidi kumi (10) kutoka miongoni mwa wawakilishi ambao wataunda:-

a. Kamati Kuu ya Baraza la Watoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika ngazi ya Taifa.
b. Kamati ya Mkoa ya Baraza la Watoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika ngazi ya Mkoa

c. Kamati ya Wilaya ya Baraza la Watoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika ngazi ya Wilaya
d. Kamati ya Kata ya Baraza la Watoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika ngazi ya Wilaya
e. Kamati ya Klabu ya Baraza la Watoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika ngazi ya Klabu pale inapoonekana inafaa.

13.3 Baada ya kuchaguliwa wajumbe wa kila kamati katika ngazi zote, wajumbe wateule watakutana siku hiyo hiyo ya uchaguzi na kuchagua miongoni mwao:-

(a) Mwenyekiti
(b) Makamu Mwenyekiti
(c) Katibu na
(d) Mweka Hazina

13.4 Katika uchaguzi wa viongozi wa Baraza katika ngazi zote uwiano wa jinsi utazingatiwa na katika ngazi ya Taifa uwiano wa uwakilishi wa wajumbe kutoka Tanzania Bara na Tanzania Visiwani pia utazingatiwa. Ili kuondoa utata, ieleweke wazi kuwa iwapo Mwenyekiti atatoka upande mmoja wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, basi Katibu itabidi atoke upande wa pili wa Muungano na kinyume chake. Katika uchaguzi wa wajumbe sita (6) wa Kamati Kuu ya Baraza la Watoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania walau theluthi moja ya wajumbe itoke kila upande wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

13.5 Baada ya uchaguzi majina ya viongozi wapya yatatangazwa katika mkutano mkuu wa ngazi husika na viongozi wapya watasimikwa kushika nafasi zao za uongozi.

13.6 Kamati Kuu itaweka miongozo na Kanuni za kuendesha uchaguzi wa wawakilishi na viongozi wa Kamati za Baraza katika Ngazi zote.

13.7 **Makabidhiano ya uongozi:** Viongozi wanaoondoka madarakani watakabidhi madaraka kwa viongozi wapya kwa kutoa taarifa ya utendaji wao uliopita kwa maandishi.

13.8 Viongozi waliochaguliwa wanaruhusiwa kutumia ubunifu wao katika kuongoza Baraza bila kwenda kinyume na Katiba hii na kwa kuzingatia misingi ya uongozi bora na demokrasia.

KIFUNGU CHA KUMI NA NNE: KAZI NA MAJUKUMU YA VIONGOZI

Baraza la Watoto la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika ngazi zote litakuwa na viongozi wafuatao ambao kazi na majukumu yao kwa mujibu wa

Katiba hii ni kama ifuatavyo kulingana na hali halisi ya mahitaji ya ngazi husika ya Baraza:-

14.1 **Kazi za Mwenyekiti**

i. Kufuatilia na kuratibu shughuli zote za Baraza.
ii. Kuwakilisha Baraza la Watoto katika mikutano mbalimbali ndani na nje ya nchi.
iii. Kuendesha Mkutano wa Baraza la Watoto.
iv. Kuwasiliana na mashirika na taasisi zinazofanya kazi za watoto au pamoja na watoto, au zile zinazoweza kusaidia masuala ya watoto ndani na nje ya nchi.
v. Kuwa Msemaji Mkuu wa Baraza la Watoto.

14.2 **Kazi za Makamu Mwenyekiti**

i. Kumshauri Mwenyekiti.
ii. Kumuwakilisha Mwenyekiti kwenye mikutano ambayo atashindwa kuhudhuria.
iii. Kutekeleza majukumu ya Mwenyekiti pale anapotakiwa kufanya hivyo na Mwenyekiti.
iv. Kutekeleza shughuli zote za Mwenyekiti endapo kwa sababu yoyote ili Mwenyekiti atashindwa kutekeleza majukumu yake.

14.3 **Kazi za Katibu**

i. Kuitisha mikutano ya Baraza la Watoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
ii. Kutoa taarifa za mikutano ya Baraza au Kamati Kuu.
iii. Kuhifadhi taarifa za mikutano ya Kamati Kuu.
iv. Kuratibu shughuli za Baraza kwa kusaidiana na Mwenyekiti.
v. Kutoa taarifa kwa Kamati Kuu kwa mikutano yote ya Baraza.
vi. Kushughulikia na kufuatilia masuala mbalimbali pale anapoombwa kufanya hivyo na Mwenyekiti.

14.4 **Kazi za Mweka Hazina**

Mweka Hazina atatekeleza kazi na majukumu yafuatayo katika ngazi husika kadri itakavyoonekana inafaa:-

i Kuwa Msimamizi Mkuu wa masuala yote ya fedha ya Baraza kwa kushirikiana na Kamati Kuu na Bodi ya Wadhamini .

ii Kuaandaa na kubuni mikakati ya kuboresha vyanzo mbalimbali vya mapato ya Baraza.

iii Kuratibu matumizi yote ya Baraza katika ngazi husika.

iv Kuandaa na kutunza taarifa zote za fedha za Baraza kwa kuweka sahihi kwa mujibu wa taratibu za utunzaji fedha na au kuhakikisha jukumu hili linatekelezwa kikamilifu na Sekretariati.

v Kuaandaa na kuwasilisha taarifa mbalimbali za fedha katika vikao na mikutano ya Kamati Kuu au Kamati ya Mkoa, Wilaya au Kata au Shehia na au katika Mkutano Mkuu wa ngazi husika.

vi Kufuatilia na kupitia mlinganyo wa mahesabu ya fedha na mali zingine za Baraza kila mara.

vii Kufanya kazi nyingine yoyote atakayoagizwa na Kamati Kuu au Mkutano Mkuu katika ngazi husika.

14.5 **Kazi za Wajumbe/wawakilishi wa mikoani:**

i. Kukusanya maoni ya wanachama wa Baraza la Watoto katika maeneo wanayoishi.
ii. Kufanya kazi sambamba na viongozi wa Serikali na Mashirika yasiyo ya Kiserikali na tasisi nyingine zinazohusika na maswala ya watoto katika kutetea na kulinda haki za watoto katika maeneo wanayoishi.
iii. Kutoa taarifa ya kina kwa Kamati Kuu ya taifa pale tukio lisilokuwa la kawaida linapotokea katika maeneo wanayowakilisha na sehemu nyinginezo.
iv. Kuelimisha jamii juu ya haki za watoto wakishirikiana na mashirika mbalimbali kama vile serikali, mashirika yasiyo ya kiserikali, mashirika ya kidini na mashirika ya kibiashara.
v. Kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa maamuzi ya viongozi wa serikali yanayowahusu watoto.
vi. Kutumia rasilimali zilizopo katika maeneo yao kwa ajili ya watoto.
vii. Kutoa taarifa kwa watoto wanaowawakilisha juu ya maamuzi ya Baraza au mambo yaliyoongelewa katika Baraza.
viii. Kufanya kazi nyingine yoyote atakayoagizwa na Kamati Kuu au Mkutano Mkuu katika ngazi husika.

KIFUNGU CHA KUMI NA TANO: VYANZO VYA MAPATO, UTUNZAJI NA MATUMIZI YA FEDHA NA RASILIMALI ZINGINE ZA BARAZA

15.1 **Vyanzo vya Mapato ya Baraza:** Baraza litakuwa na vyanzo vifuatavyo vya mapato:-

i. Wafadhili mbali mbali ambao watakuwa ni watu binafsi, mashirika yaliyo ndani ya nchi na yale yaliyo nje ya nchi.
ii. Michango mbalimbali ya fedha na/au mali kutoka kwa watu binafsi na makampuni na wasamaria wema.
iii. Uwekezaji, hisa na
iv. Vyanzo vingine halali

15.2 Fedha au michango kwa Baraza zitaombwa au kupatikana baada ya Kamati Kuu kuridhia.

15.3 Baraza pia litapendekeza shughuli au miradi mbalimbali ambayo itarahisisha upatikanaji wa vyanzo vya fedha kwa ajili ya maendeleo ya Baraza.

15.4 **Matumizi ya fedha na rasilimali za Baraza:** Fedha na rasimali nyingine za Baraza zitatumika kwa ajili ya kutekeleza shughuli za Baraza tu.

15.5 **Utunzaji wa fedha na rasilimali za Baraza:** Fedha na rasilimali za Baraza zitatunzwa kulingana na utaratibu unaokubalika kitaalamu na kumbukumbu zitawekwa kwa shughuli zote kwa muda wa mwaka mzima.

15.6 Mwaka wa fedha wa Baraza utaanza Januari na kuisha Disemba kila mwaka.

15.7 Kumbukumbu za fedha na rasilimali zingine zitawasilishwa kwa mkaguzi wa mahesabu mwenye sifa na aliyeandikishwa ili ayakague na kutoa taarifa ya kitaalamu walau mara moja kwa mwaka.

15.8 Fedha za Baraza zitatunzwa ama katika akaunti zitakazofunguliwa kwa jina la Baraza au kwenye akaunti za taasisi wadhamini kwa makubaliano maalum ya maandishi.

15.9 Fedha zote zitawekwa Benki isipokuwa kiasi kidogo kitakachokubaliwa na Kamati Kuu kwa ajili ya kulipia gharama za kila siku pale inapoonekana inahitajika kufanya hivyo.

KIFUNGU CHA KUMI NA SITA: MUUNDO WA UONGOZI KATIKA BARAZA LA WATOTO LA JAMHURI YA MUUNGANO KATIKA NGAZI YA MKOA, WILAYA NA KATA AU SHEHIA

16.1 Katika ngazi ya Mkoa au Wilaya au Kata Baraza la Watoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania litakuwa na vyombo vifuatavyo:-

(a) Mkutano Mkuu wa wa Kata au Shehia, Wilaya au Mkoa wa Baraza
(b) Kamati ya Kata au Shehia, Wilaya au Mkoa ya Baraza
(c) Mshauri au Washauri wa Baraza wa Wilaya au Mkoa na au Kata au Shehia
(d) Mlezi au Walezi wa Baraza la katika Wilaya au Mkoa na au Kata au Shehia

16.2 Utaratibu wa uchaguzi na uendeshaji wa vyombo hivi utalandana na mfumo ulioelezwa katika vifungu vilivyotangulia vinavyohusu ngazi ya Taifa.

16.3 **MKUTANO MKUU WA BARAZA KATIKA MKOA AU WILAYA, KATA AU SHEHIA**

16.3.1 Kutakuwa na Mkutano Mkuu wa Baraza katika Wilaya au Mkoa au Kata au Shehia husika utakaofanyika mara moja kwa mwaka.

16.3.1.1 Mkutano Mkuu utakuwa ndicho chombo cha juu zaidi na cha mwisho katika kufanya maamuzi juu ya maswala mbalimbali ya Baraza katika Ngazi ya Wilaya au Mkoa na au Kata au Shehia.

16.3.1.2 Mkutano Mkuu wa Ngazi ya Wilaya au Mkoa au Kata au Shehia utafanya shughuli zifuatazo:-

(a) Kupokea, kujadili, kukubali au kukataa taarifa ya maendeleo na utekelezaji wa shughuli za Baraza katika Ngazi ya Wilaya au Mkoa au Kata au Shehia kila mwaka.
(b) Kupitisha mpango kazi na bajeti kwa mwaka unaofuata katika Ngazi ya Wilaya au Mkoa.
(c) Kufanya uchaguzi wa wawakilishi wa kutoka katika Mkoa husika watakaokuwa wawakilishi katika Baraza la Watoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(d) Kujaza nafasi za uwakilishi katika Baraza la Watoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, iwapo kwa sababu yeyote ile nafasi ya mwakilishi imekuwa wazi.
(e) Kuwajibisha wawakilishi au viongozi katika Ngazi ya Wilaya au Mkoa husika.
(f) Kupokea na kuthibitisha wanachama wapya katika Wilaya au Mkoa husika.
(g) Kuwajibisha wanachama waliokiuka malengo, madhumuni, Katiba na maadili ya Baraza katika Wilaya au Mkoa husika.
(h) Kutoa maelekezo juu ya mipango, mikakati na utekelezaji wa mamlaka na shughuli za Baraza katika Wilaya au Mkoa husika.
(i) Kufanya Uchaguzi wa viongozi wa Barza katika Wilaya au Mkoa.
(j) Kupokea maombi ya wanachama wapya, kuyajadili na ama kuyakubali au kuyakataa.
(k) Kufanya jambo jingine lolote ambalo kwa kawaida hufanywa na Mkutano Mkuu wa Baraza katika Wilaya au Mkoa husika

16.4 **Kamati ya Baraza :** Kutakuwa na Kamati ya Mkoa au Wilaya ya Baraza ambayo itakuwa na majukumu ya kuratibu na kusimamia shughuli za Baraza katika eneo husika.

16.5 **Mshauri au Washauri wa Baraza Mkoa au Wilaya:** Baraza katika ngazi ya Wilaya au Mkoa litateua ama Afisa Maendeleo ya Jamii katika Ngazi husika kwa Tanzania Bara au Afisa Wanawake na Watoto kwa upande wa Tanzania Visiwani na au afisa mwingine yeyote mwenye utaalamu wa kumwezesha kulishauri Baraza katika ngazi husika.

16.6 **Mlezi au Walezi:** Baraza linaweza kuwa na Mlezi au Walezi wa Baraza katika ngazi mbalimbali kama ilivyoelezwa.

KIFUNGU CHA KUMI NA SABA: MUUNDO WA UONGOZI KATIKA KLABU ZA WATOTO MASHULENI NA SEHEMU NYINGINEZO

17.1 Baraza linaweza kuanzisha Klabu za watoto katika mashule na sehemu mbalimbali ambazo kuna jumuiko la watoto wasipungua kumi (10).

17.2 Uongozi wa Klabu ya Watoto utakuwa na Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Katibu na Mweka Hazina na pale inapoonekana inafaa wajumbe wasiozidi sita.

17.3 Jukumu la Klabu za Watoto litakuwa ni kuunganisha watoto na kuratibu shughuli mbalimbali za Baraza katika eneo lao.

17.4 Klabu yaweza kumteua mwalimu au mtu mwingine inayeona anafaa ili awe mlezi au Mshauri wa Klabu husika.

17.5 Klabu zitaongozwa na Kanuni na Taratibu zitakazowekwa na Kamati Kuu.

KIFUNGU CHA KUMI NA NANE: MLEZI AU WALEZI WA BARAZA

18.1 Baraza la Watoto la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linaweza kuteua taasisi au mtu au watu wowote kuwa Mlezi au Walezi wa Baraza katika Ngazi mbalimbali za Baraza.

18.2 Mlezi atakuwa ama ni taasisi inayojishughulisha na maswala ya watoto au ni mtu mashuhuri na mwaadilifu mwenye sifa na mchango mkubwa katika kujihusisha na shughuli za kuhudumia na kuendeleza jamii.

KIFUNGU CHA KUMI NA TISA: KUVUNJWA KWA BARAZA

19.1 Baraza litavunjwa endapo robo tatu ya wajumbe wote wa Baraza watapiga kura kuamua hivyo.

19.2 Uamuzi wa kulivunja Baraza kwa kupiga kura utafikiwa baada ya majadiliano ya pamoja ya Kamati Kuu, Washauri, Walezi, Wafadhili na Wadhamini wa Baraza kulinusuru Baraza lisife kushindikana.

19.3 Baraza litakapovunjwa madeni yake yote yatalipwa, na rasilimali zitakazobaki zitagawanywa kwa Baraza lingine, shirika au chama chochote Tanzania ambacho kinamtazamo unaofanana na wa Baraza.

19.4 Kazi ya kulipa madeni na kukabidhi rasilimaili za Baraza lililovunjwa itafanywa na wadhamini kwa kufuata sheria husika za nchi.

19.5 Fedha na rasilimali za Baraza haziwezi kugawawiwa kwa wajumbe, washauri/walezi au wadhamini.

KIFUNGU CHA ISHIRINI: MENGINEYO

20.1 MAREKEBISHO YA KATIBA

20.1.1 Katiba hii inaweza kurekebishwa baada ya makubaliano ya robo tatu (3/4) ya wajumbe wote wa Baraza pamoja wanaohudhuria na kupiga kura katika Mkutano Mkuu.

20.1.1 Mabadiliko ya Katiba yatawasilishwa kwa maandishi kwa Kamati Kuu, Bodi ya Ushauri, Bodi ya Wadhamini, Mlezi au Walezi na mamlaka ambako Baraza limesajiliwa.

20.2 **LAKIRI YA BARAZA**

20.2.1 Kutakuwa na lakiri au mhuri wa Baraza la Watoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itakayotumika kwa kuthibitisha uhalali wa nyaraka zote muhimu za Baraza.

20.2.2 Lakiri ya Baraza itawekwa kwenye nyaraka muhimu za Baraza chini ya mamlaka ya Kamati Kuu tu.

20.2.3 Kila nyaraka muhimu itakayowekwa lakiri itasainiwa na Mwenyekiti na au Katibu.

KUTUMIKA KWA KATIBA HII

---

*Katiba hii imepitishwa na Mkutano Mkuu uliofanyika leo tarehe **18** Mwezi **Januari** .Mwaka **2008** .katika Ukumbi wa **IFISI COMMUNITY CENTRE (ICC)** hapa **MBALIZI, JIJINI MBEYA** . na itaanza kutumika rasmi kuanzi leo hii.*

....

MWENYEKITI **KATIBU**